



# PAMBANO LILIOFICHIKA

Jumbe tatu zenye ufunuo...





## Uchangukaji wa jamii...

Vita na misukosuko, vurugu na mauaji, njaa na dhiki, Vibunga, ghalika, matetemeko ya ardhi...haya si matukio mapya.

Hata hivyo, kizazi kilichoko leo kinakabiliana na changa moto mpya na ngumu; nazo ni matatizo ya kimazingara, uhandisi wa kinasaba, mabadiliko katika hali ya anga, magojwa yanayo husiana na chakula, na kadhalika. Wengi wetu pia tutaweza kutambua ya kwamba jamii yetu inajitenga na maadili fulani ya kitabia ambayo ni ya kimsingi



Usalama...  
Uaminifu...  
Uhakika...  
Utunzaji...  
Upendo...

Wengi wamebaki  
huku wakijihisi  
kuwa wadogo na  
wanyonge, lakini  
je, si ingetupasa sis  
kujiuliza swali hili:



Haya yote  
yatendeka kwa nini.



Kunayo sababu ya mabadiliko haya. Habari njema ni kwamba kunalo pia suluhisho.

Hatuzungumzii ile aina ya utatuzi ambayo siku hizi hupendekezwa na wanasiasa au viongozi wa kidini. Historia yaonyesha kuwa mara nyingi, walio wengi ndio hukosea, na pia, japokuwa kumefanywa mikataba mingi ya amani, masikilizo ya kuushirikiana pamoja na mipango yenye makusudi mema, hali kadhalika tamaa ya uongozi na ile tamaa idumuyo ndani ya moyo wa binadamu, hali yote hayatatoweka.

Kama vile mataifa yanavyo ungana kisiasa, kijeshi na yanaonekana kiuchumi, vivyo hivyo twaona ya



## Siku za usoni zitatuletea yapi?

kifanyika kidini. Yale yanayoendelea ni mapambano kati ya mema na mabaya, lakini yatakoma. Nyuma ya ukweli huu unaohusu misukosuko, kuna mpango unaotekelezwa.

**Kitabu cha vitabu, yaani Biblia, kinalo jambo la kusema kuhusu hali ya maisha ilivyo. Hasa ina kuongelesha wewe unayetafuta maelezo kamili wewe unayetaka kuyajua mambo yajayo.**

**Kufikia sasa, unabii wa biblia haujawahi kufeli. Kwa hivyo, twaamini kuwa unabii wa siku za mwisho utatimia pia.**

**Katika kitabu cha Ufunuo, twaupata mfululizo wa unabii unaoendelea kutimia sasa. Tutauangalia unabii huu kwa undani.**



# Ujumbe wa kwanza

***Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji.***

*Ufunuo 14: 6-7*

Waweza kuusoma ujumbe wa kwanza katika ukurasa unaofuata.

Yasema kuwa jumbe tatu hizi zapeanwa na malaika. Neno la kiyunani litumikalo kumaanisha malaika ni “angelon”, maana yake mjumbe. Hivyo basi malaika hawa watatu husimamia waume na wake watendao kazi kulingana na mapenzi ya Mungu, na ambao watapeana ujumbe huu, ambao ni “injili ya milele” wa ulimwengu, kwa nguvu zao zote.

## INJILI YA MILELE

Je, “injili ya milele” ni nini? Jawabu limeelezwa kwa kinaganaga kwenye Biblia, katika injili ya Yohana 3:16 Hapo husema hivi;

**“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.” (Johana 3:16)**

Sote twaifahamu hadithi ya Biblia kuhusu Adamu na Hawa, ambao walikosa kutii na kulila tunda lililo katazwa, walikuwa tayari wamelipokea onyo, na walijua ya kwamba wangepariki nyuma ya hadithi hii inayoonekana kuwa rahisi, umefichika mkosi ambao tayari umewafikia binadamu wote, Biblia yahakikisha kuwa mshahara wa dhambi ni mauti (Warumi 6:23), na hapa huzungumzia mauti ya milele, Mungu, ambaye ndiye muumbaji wetu, ndiye chanzo cha uhai wote, hivyo basi wakati mababu zetu walipoamua kuyapuuza maonyo ya Mungu, walimwacha yeye

ambaye ndiyehai. Lakini Mungu humpenda binadamu.

Yeye aliamua kujitwalia hukumu ya kifo inayotufaa juu yake. Alimtuma mwanawe, Yesu Kristo, ambaye alikuwa tayari kuyapitia mateso badala yetu sisi.

Japo Yesu alikuwa ni Mungu, alikuja kama binadamu (Yohana 1:13,14 na Wafilipi 2:5-8). Akiwa kama binadamu, ingempasa ajaribiwe kwa njia zote kama vile sisi. Na kwa vile angeichukua nafasi yetu, ingekuwa tu ni kwa kuishi maisha ya haki, pasipo dhambi, ili aweze kujitwalia adhabu yetu bila yake mwenyewe kuwa na hatia. Kristo aliyashinda majaribu YOTE kupitia kwa nguvu za Mungu (Wahibirania 2:17-18).

Ni yeye pekee aliyeyatenda haya



(Warumi 3:23). Hatimaye, aliutoa uhai wake msalabani ili atuweke huru wewe na mimi kutokana na mauti ya milele. Husema hivi:

**“Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo.” (Waebrania 9:22)**





Kwa hivyo, ni juu yako wewe nami tulipokee toleo hili la Kristo kwa imani. Kama wajiona kuwa ni mwenye dhambi, waweza kujiondolea mzigo huo wa dhambi kwa kumjia Kristo. Biblia yasema:

**“Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.”**

*(1 Yohana 1:9)*

Kila mmoja wetu anayekubali kuhesabiwa haki kwa imani ataokolewa. Je, sihizo ni habari njema?

### MCHENI MUNGU NA KUMTUKUZA

Lakini maisha hayakomi wakati tunasema NDIYO kwa Yesu. Hapo, maisha yetu pamoja na Kristo huanza. Ndipo itakaponekana maishani mwetu kuwa tumepitia kwenye mabadiliko. Biblia yasema kuwa tutabadilishwa kwa kuwa na mageuzi kamili ya nia (Warumi 12:2). Haya ndiyo yanayotendeka pale tusemapo NDIYO kwa Yesu, Roho mtakatifu akishaingia mioyoni mwetu. Hapo ndipo tutakapoyafuata maagizo ya Mungu, wala sio njia zetu wenyewe, huku tukiwezesha na Roho mtakatifu. Hatimaye sifa za kitabia

kama vile upendo, furaha, amani, wema na urafiki zitajitokeza maishani mwetu, badala ya chuki, hasira na tamaa... (Wagalatia 5:16-26). Jambo hili hatuwezi kulitimiza peke yetu, bali ni kwa msaada wa Mungu. Kwa hivyo, maana yake kumtukuza Mungu ni kushuhudia tabia yake ndani ya maisha yetu, na kwa njia hii kumfanya ajulikane kwa wale wanaotuzunguka. Yesu ametupa mfano, na sasa ni juu yetu, - huku tukisaidiwa na Mungu – kuiendeleza kazi yake kwa kuidhihirisha tabia yake katika maisha yetu na mafundisho yetu (1 Petero 2:21, na Waefeso 3:10).

Kuishi pamoja na Kristo na kudhihirisha tabia yake maishani mwetu hushirikisha mambo mengi. Yesu asema hivi:

**“Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuata”. Na pia “Mkinipenda mtazishika amri zangu.”**

*(Mathaya 16:24 na Yohana 14:15)*

Mtu aliyempokea Yesu kwa imani watafurahia kuzifuata amri zake. Amri za Mungu ametupa amri hizi kumi ili tufahamu jinsi tutakavyoimarisha uhusiano wetu na Mungu, hali kadhalika sisi kwa sisi. Katika barua ya kwanza ya Yohana, twajaribiwa hivi:



**“Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu.”**  
(Matendo 1:8)

Nguvu hizo hizo twaweza kuzipata pia. Kwa hivyo, kama vile ingempasa Yesu kupewa nguvu za kuzishinda dhambi na Mungu, vivyo hivyo nasi pia twaweza kuyashinda majaribu yote yanoyotukabili (Yohana 5: 30 na 1 Wakorintho 10: 13). Mfuasi wa Kristo atakuwa sio tu msikilizaji wa neno, mbali pia mtendaji. Imani ya kweli hudhahiliwa kwa vitendo. Maisha au vitendo huambatana na mapenzi ya Mungu. (Yohana 1:22 na 2:14-26, pia 1 yohana 2:29).

Biblia yadhiihiliwa kuwa roho mtakatifu atapeanwa kwa wale wanaomtii Mungu (Matendo 5:32), na kuwa Roho Mtakatifu ndiye atuwezeshaye kuishi bila kutenda dhambi. Biblia yaahidi hivi:

**“Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu.”** (1 Yohana 3:9; na 2 Petro 1:4)

Tukishaiamini ahadi hii, tutapata kuwa twaupokea usaidizi wa kulishinda kila jaribu litakalotukabili.

Twatumai kuwa utaupata uzoefu huu unaohusu kushirikiana kwa nguvu za kibinadamu na za kiungu, kwani hili ni jambo ambalo yatupasa sisi sote kulifanya ili tumheshimu Mungu katika shughuli zetu

**“Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake. Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake. Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda.”**

(1 Yohana 2:3-6)

K wa hivyo, kumwogopa Mungu humanisha pia humtii Mungu.

Tukishaelewa kwa undani yale yote ambayo Mungu ameyatoa kafara ili kutuokoa sisi, itakuwa ni furaha kwetu kuzifuata amri za Mungu. Kuwa chini ya sheria hakutakuwa tena ni utumwa, bali tutatii kutokana na upendo pamoja na shukrani kwa Mungu aliyetupenda kwanza.

Yesu alipokuwa akipaa mbinguni, aliwaambia wanafunzi wake:





mbali mbali maishani.

“Lakini” huenda utauliza, “ikiwa utausahau msaada wa Mungu na kuanguka majaribuni, la kufanya ni nini?” Basi hapo, sisi ndio tutakaokuwa tumeusahau msaada wake, wala si yeye. Hapo litakuwa ni jambo la muhimu kwetu sisi kumrejea Yesu na kushikamana naye. Atakuwa tayari zaidi kutupokea na kumsamehe kila mwenye dhambi anayetubu. Roho Mtakatifu atatutembelea ili atusaidie kuzikubali dhambi zetu, kuzitubu, kuomba msamaha na kuupokea wokovu wa yesu Kristo tena. Kama Biblia inavyosema:

**“Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote.”** (1 Yohana 2:1-2)

Haya yamekuwa ni maneno ya kuchangamsha. Ikiwa wewe ni mmoja wao, yakupasa ujue kuwa yesu huwa tayari kukupokea wakati wowote. Lakini hamna njia nyingine ya wokovu. Ni lazima sisi zote tupitie kwa Yesu ili tuokolewe. Hivyo basi Yesu asema:

**“Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele.”** (Yohana 14:6)

Kwa hivyo, kuihubiri “injili ya milele” na “kumheshimu Mungu” hujumuisha siyo tu kumpokea Yesu kama mwokozi wetu binafsi wakati mmoja fulani maishani, mbali pia tutayaishi maisha yetu tukiwa pamoja na kristo, na kuidhihirisa tabia yake maishani mwetu. Tunaposhirikiana na nguvu za mbingu kwa jinsi hii, basi tutaupokea msaada tunaouhitaji ili kuwa mshahidi walio hai kwake, na kwa neema yake tutakuwa tayari wakati Yesu atakuja hivi karibuni kuwachukuwa walio wake.



Biblia pia yatuhimiza tumheshimu Mungu kwa miili yetu. Katika 1 Wakorintho 6:19, husema:

**“Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe.”** (1 Wakorintho 6:19-20)


Je, si hili ni jambo la kutuamsha mawazo, ya kuwa miili yetu yalinganiswa na hekalu? Katika agano la kale, hekalu lilikuwa wakfu kwa Mungu. Kadri tuwezavyo, na huku tukiwezeswa na Mungu, ni lazima tujaribu kuutunza mwili huu wa kupendeza ambao Mungu ametupa. Ni lazima tuzirudie tiba za kiasili: yaani hewa safi, mwanga wa jua, mazoezi ya viungo, chakula chenye afya bora, usafi, usingizi na pumziko la kutosha, na kumtengemea Mungu.

Hapo tutakuwa na maisha bora ya kimwili, kimawazo na kiroho.

Kule kuutunza mwili vyema kadri tuwezaavyo ni njia moja pia ya kumtukiza Muumbaji wetu, jambo ambalo yampasa kila mfuasiwa wa Kristo kulizingatia.

Sasa tutaitazama sehemu ya pili ya ujumbe huu wa kwanza, ambao leo wafaa kutangazwa kwa sauti ya juu:

## Majuma 70 = Miaka 1810



## Siku 2300 = Miaka 1810

### SAA YA HUKUMU YAKE IMEFIKA

Biblia yasema kuwa kabla ya kurudi kwake Yesu Kristo, itakuwa tayari imeamuliwa ni akina nani watakaookolewa na watakaopotea. Kusema kweli, sisi ndio tunaoamua ni kikundi gani tutakachojiunga nacho. Biblia yatuambia ya kwamba Yesu leo ni kuhani mkuu katika hekalu ya mbinguni, ambapo anatumia upatanisho mbele za Mungu. Ili tuweze kuielewa huduma anayotufanyia huko, tumeupokea mfano ambao tunaweza kuutafakari: nalo ndilo hekalu la hapa duniani, ambalo habari zake twaweza kuzisoma kwenya Agano Jipya. Paulo huiita “nakala au kivuli cha mambo ya mbinguni (Waebrania 8:5). Ulikuwa tu ni mfano mdogo wa hekalu ya mbinguni. Waweza kuyasoma haya katika aya ya 8 na 9 ya Waebrania.

Katika chumba cha kwanza cha hekalu ya duniani kuhani alihudumu kila siku. Chumba hiki kilijulikana kama “pahali patakatifu” (Walawii 4). Mwishoni mwa mwaka wa hekalu-yaani mara moja kwa mwaka-katika “Siku kuu ya Upatanisho,” kuhani alienda kwenye chumba cha pili; yaani “Pahali Patakatifu Mno,” (Waebrania 9:7). Katika huduma ya hekalu wakati wa Agano la kale, walikuwa wameshazihamisha dhambi zao kwa mfano (kupitia kwenye

damu ya mnyama anayetolewa kafara) hadi kwenye hekalu. Katika siku hii ya kipekee; yaani “Siku kuu ya Upatanisho”, ilibidi hekalu lisafishwe kutokana na zile dhambi zilizohamishiwa huko. Ilikuwa ni siku ya hukumu. (Hebu soma Walawii 4 na 16). Dhambi ilisafishwa kwa njia ya mfano toka ndani ya hekalu, na muda usio mrefu baadaye wangeweza kuiadhimisha sikukuu iliyofuata, ambayo ndiyo sikukuu ya Tabenakulo. Sikukuu ya Tabenakulo ilikuwa ni sherehe ilyojumuisha hali ya furaha na kutoa shukrani.

Kwa vile huduma ya hekaluni wakati wa Agano la kale ilikuwa ni mfano tu wa yale ambayo Yesu angeyafanya baadaye katika hekalu ya mbinguni, ni jambo dhahiri kuwa lazima pia kutakuwepo na siku ya hukumu kabla ya “sikukuu ya furaha” ambayo itafanyika pale Yesu atakapoungana na watu wake.

***Nabii Daniel atujulisha kuhusu hii sikuya hukumu-huku “kusafishwa”- au kuhesabiwa haki - kwa hekalu ya Mbinguni.***

Katika kitabu cha Danieli, aya ya 8, fungu la 14, twaambiwa kuwa wakati ambapo tendo hili la hukumu lingeanza ulikua tayari



1844  
po Kr.



**1844 AD  
Hukumu  
yaanza  
mbinguni**

**Saa ya  
hukumu  
imefika**

**Kurudi kwa  
Yesu**

umeshapangwa.

Haya yaambatana na kichwa chetu "saa ya hukumu Yake imewadia" Je, "saa" muda huu wa kipekee utafika lini? Danieli aliarifiwa kuwa siku 2300 zingepita kwanza; kisha hukumu hii ingeaza.

***Kwa lugha ya kinabii, siku moja – mwaka mmoja (Ezekiel 4:6), kwa hivyo hapa twaazungumzia muda mrefu unaojumuisha miaka 2300.***

Baadaye kidogo katika kitabu cha Daniel, twapata kujua ni wakati gani unabii huu ungeanzia (soma Daniel 9:25) nayo historia yatarifu zaidi kuwa tukio ambalo lingeuhibitisha mwanzo huu lilifanyika wakati wa kupukutika kwa majani, mnamo mwaka wa 457 BC.

Hivyo basi tukihesabu miaka 2300 toka wakati huo (bila kuhesabu mwaka wa sifuri), twafikia kati ya miaka ya 1840. Kulingana na unabii, ni wakati huu ambapo "sikukuu ya upatanisho" ingeanza huko mbinguni.

Biblia yasema kuwa hukumu itaanza kwa wale waliojitolea kuwa wana wa Mungu. (1 Petero 4:17). Majina yao yatachunguzwa, nayo maisha yao yatajaribiwa kwa mujibu wa mwanga utokao kwenye sheria ya Mungu ambayo hupatikana kwenye chumba cha pili cha hekalu, yaani "pahali patakatifu mno"

(Waebrania 9:3-4).

Wakati wa Agano la kale, ili walazimu kuziungama dhambi zote kabla ya sikukuu ya upatanisho, ili waweze kupatanisha.

***Vivyo hivyo, yatupasa nasi kuzianika dhambi zetu zote mbele za Mungu, ili Yesu atupatanishe. Wakati ambapo "siku ya hukumu" itakwisha huko mbinguni, nao muda wetu wa neema utakuwa umekwisha.***

Haya yatatokea muda kidogo kabla ya kurudi kwake Yesu kama bwana na mwokozi wetu. Damu ya Yesu itakuwa imeweza kuwasafisha wale tu ambao watakuwa wameomba wapewe, yaani wale walioupokea msamaha kupitia kwa Yesu Kristo. Wengine wote watapotea. Japo Yesu alitamani kuwaoko pia, hawa kuipokea zawadi ya wokovu. Siku moja watakuwa wame chelewa, na japo Mungu atawalilia, hata hivyo ili kuzingatia haki itawalazimu wahukumiwe kulingana na matendo yao.

Imeandikwa kuwa hao watateketezwa kwa moto na salfa (Ufunuo 20: 12 na 21:8).

Yesu sasa yu mbinguni (Yohana 14:1-3, na Matendo 1:8-11). Yesu ndiye mkombozi na mwokozi, lakini pia ndiye hakimu. Yeye ndiye huamua ni nani atakayeokolewa na ni nani atakayepotea. Kwa hivyo wajua ya

kwamba hukumu itapitishwa kwa haki. Njia moja tu ya kupitia kwenye hukumu hii ni kuzieleza dhambi zetu juu ya Yesu.

Hakuna ajuaye ni lini Yesu ataimaliza hiyo huduma yake ya kuitekeleza hukumu kama kuhani mkuu huko hekalluni. Hapana pia ajuaye ni lini uhai wake utakoma. Kwa hivyo, hatuna muda wa kupoteza. Siku ya neema ni sasa. Sasa ndio Mungu anapokuita unyenyekee na kuziweka dhambi zako zote miguuni pake Yesu.

kwanza ambao sasa utatangazwa kwa sauti kuu, ya sema:

MCHENI YEYE ALIYEUMBA MBINGU NA NCHI,  
NA BAHARI, NA CHEMCHEMI ZA MAJI

## ...saa ya hukumu yake imefika...

**“Wote anipao Baba watakuja kwangu; wala ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe.”**  
*(Yohana 6:37)*

Yeye yu hivyo. Waweza kumjia wakati wowote. Atakupokea na kukupa amani, yaani amani yake, amani na usalama ambazo dunia kamwe haiwezi kukupa! (Yohana 6:37), Je, ungependa kulikubali toleo hili? Ni juu yako, lakini yakupasa ujue kuwa kamwe hautajuta ikiwa utajibu NDIYO kwa hili toleo, kumbuka maneno ya Biblia.

**“Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli.”** *(Yohana 8:36).* **“Walakini alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru.”**  
*(2 Wakorintho 3:17)*

Hebu na tu siwe watumwa wa kumtumikia shetani pamoja na ule mzigo wa dhambi ulioko maishani mwetu. Lakini, huku tukisaidiwa na Mungu, hebu na tuzikate kamba ili tuwe huru ndani ya Kristo. Hapo tutakuwa tumehama toka mautini hadi uzimani. Hebu na tuikate kauli hii sasa, ikiwa ingali siku ya neema. (mengine zaidi kuhusu ujumbe huu yapatikana kwenye kitabu kiiwacho “Vita Kuu”).

Sehemu ya mwisho ya ujumbe huu wa

Biblia yatuambia ya kwamba Mungu aliziumba mbingu na nchi, bahari na vyote vilivyomo kwa siku sita, akastarehe siku ya saba. Naye Mungu akaibariki siku ya saba, akaitakasa (Mwanzo 2:1-3), katika amri ya nne kwenye Biblia, kutoka sura ya 20 mafungu ya 8-11, twaipata amri kuhusu siku ya kustarehe. Hapo twayapata mawaidha hayo ya kumcha muumbaji. Siku ya pumziko ambayo Biblia huita Sabato, imetengwa ili sisi tuweze kupata nafasi ya kumwabudu, kumwinua na kunjua mwumbaji wetu kwa njia ya kipekee. Tutamjua Mungu vyema zaidi kwa kulisoma Neno lake na pia kwa kuutafakari uumbaji wake. Japokuwa uumbaji huu sasa waendelea kuharibiwa, bado kunavyo vitu vingi vya kupendeza vinavyotuzingira. Kadri tunavyoendelea kujifundisha mengi zaidi kuhusu uumbaji wa Mungu, ndivyo tutakavyozidi kumtamani muumbaji.

Bila shaka kunavyo vitu vingi vya kupendeza kwenye uumbaji hivi kwamba mtu hupata yamempumbaza kabisa.

Hebu litazame ua, au mdudu, na mbwa, au binadamu, vyote vimeundwa vyema na ifaavyo.







## ...Msujudieni yeye...

Ni jambo la kuhuzunisha ya kwamba watu wengine wameanza kuwa na tashwishi kama kweli mungu ndiye muumba. Mnamo karne ya 19, Charles Darwin alilitangaza pendekezolake kuhusu chanzo cha viumbe.

Kwa bahati mbaya, wengi wameiamini nadharia hii ya kibinadamu ya mageuko kutoka sahili kuwa tata, ambayo mara kwa mara hujipenyeza kwenye vitabu na majarida mengine yanayo somwa shuleni na vyuoni.

Hebu tusimwinue binadamu na nadharia zake za kupotosha zinazohusu mwanzo wa uhai, bali tumwinue na

kumsujudu muumbaji alieumba siku sita na kustarehe siku ya saba miaka 6000 iliyopita Ametuambia sisi vitu vipendezavyo ajabu.

Ikiwa bado unayo mashaka kama kweli Mungu ndiye muumba, hebu yafumbe macho yako kwa siku nzima ili uelewe jinsi macho yako husaidia katika yote uyatendayo. Kwa njia hii, twaona kuna viungo vyetu vyote ni muhimu kwetu kwa kuyafanya mambo ifavyo. Hatimaye, hebu na tumshukuru Mungu/ Yesu Kristo kwa uhai wetu. Biblia yasema hivi:

**“Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye.”** (Wakolosai 1:17; Yohana 1:1-3; Na mwanzo 1:26).

Kama kila mtu angalipata nafasi ya kumsujudu Mungu katika ile siku ambayo yeye alitenga ili itumiwe kwa utakatifu, hakungekuwa na watu wenye nadharia ya mageuzi na wale wasioamini kwamba kuna Mungu. Mungu anao utajiri wa mibaraka kwa wale wanaomsujudu kwa Roho na kweli.

# Ujumbe Wa pili

**„Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanyweshwa mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake“**

*Ufunuo 14:8*

## AMEAGUKA, BABULONI AMEAGUKA

Ni nani “Babuloni”, “Babuloni Mkuu” na “Kahaba”?

Katika Ufunuo sura ya 17, “kahaba” ameelezwa. Anazo sifa nyingi zilizoeleza, hivyo itakuwa ni rahisi kumtambua. Usikiapo jambo hili mara ya kwanza, huenda ukaichukulia hii kuwa ni lugha kali, lakini hata hivyo: alama zote za kutambulisha katika Biblia zaingiana na Kanisa Katoliki. Bila shaka kuna washiriki wengi wa kanisa hili ambao ni wazuri, wasio na hatia, na si kusudi letu kuwanasa. Lakini twajihisi kuwa tunao mwito wa kuwaonya wao, pamoja na wengineo dhidi ya mfumo huo, hali kadhalika mafundisho ambayo mfumo umejengwa juu yake. Usuli ya onyo hili ni amri ya Biblia, na pia ya kwamba hatuwezi, hali kadhalika kwa sababu ishara na alama za kumtambua yule “Kahaba” kwa mujibu wa biblia zaingiana na utawala huu (Ufunuo 17:5).

Mojawapo ya ishara hizi ni:

**“Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, la siri, Babeli mkuu, mama wa makahaba na machukizo ya nchi.” (Ufunuo 17:5)**

Kanisa katoliki hujiita mama wamakanisa. Katika barua waliotumiwa maaskofu wote wa ulimwengu, Cardinal Joseph Ratzinger aliandika hivi:

“Yapasa izidi kueleweka waziwazi ya kwamba kanisa moja lilio takatifu, la kikatoliki na la mitume linalozaa dunia nzima, hilo sio dada bali ni mama wa makanisa yote” (Daily telegraph, September 4, 2000).

Matangazo ya aina hii huchangia

kuhakikisha ya kwamba kanisa katoliki ndilo linalo utimiza unabii wa Ufunuo 17:5.

Ujumbe wa pili umeeleza pia hali ya kuogofya katika ulimwengu wa kidini. Biblia ya funua kuwa yule “kahaba” au “Babeli Mkuu”, ata utongoza ulimwengu kupitia kwenye mafundisho yake yasiyo ya kibiblia, yaani ule mvinyo wake unaolevya. Pengine udanganyifu mkuu sana ambao kanisa katoliki imewahi kuufanya kwa miaka mingi ni kule kuzibadilisha amri kumi za Mungu kama tuzisomavyo katika Kutoka aya ya 20, mafungu ya 3-17. Kwa bahati mbaya, makanisa ya Lutheri yamezikubali amri hizi bandia kwenye katekismus zao, nao wamewatongoza watu kwa amri hizi bandia. (Tutayajadili haya baadaye chini ya kichwa hiki. “Mhuri wa Mungu na alama ya mnyama”).

## MVINYO WA BABELI UNAOLEVYA

Kanisa katoliki, yaani yule “kahaba” (Ufunuo 17:5) pia limeyatanguliza mafundisho mengine mengi yasiyo ya Biblia, kama vile ibada ya Bikira Mariamu, Hali kadhalika fundisho la kutokufa kwa Roho ya binadamu, ambalo pia hupatikana kati ya mafundisho ya Kizazi Kipya na ya wanaoamini katika kuwasiliana na mapepo. Leo hii, makanisa kadhaa wameyakubali mafundisho yanayohusu mawasiliano ya mapepo. Imani hii ya mizimu huyafungulia mlango mapepo yatakayo kupoteza, kwa mafundisho ambayo chanzo chake ni zile nguvu za uovu. Adhari za malaika waovu zitaendelea kubainika katika makanisa tofauti tunapokaribia mwisho wa nyakati (Kumbukumbu 18:10-12, na 2 Wathesalonike 2:9). Soma zaidi kuhusu haya kwenye kijitabu kiitwacho “Vizuka vya



Mariamuu".

### Komunyo

Kanisa katoliki hufundisha kuwa mkate na divai hubadilika na kuwa mwili na damu ya Yesu hasa, wakati ambapo kuhani huviinua na kuvibariki, na ya kwamba wao humtoa kafara ("humwua") Yesu upya

walao mkate na kunywa divai. Kwa hivyo hujulikana kama kafara ya misa takatifu. Hii ni mojawapo ya ibada zinazoundhi ambazo kanisa katoliki imezitanguliza. Kinyume na hayo, Biblia husema kuwa Yesu alitolewa kafara mara moja, na kwamba komunyo utakuwa ni ukumbusho wa yale aliyoyatenda Yesu ili atuokoe (Waebrania 9:24-28 na/Wakorintho 11:23-26)

Kunazo ishara nyingi zinazoonyesha kuwa waprotestanti walioasi pia wata ikubali komunyo hii ya kikatoliki hivi karibuni.

### Maazimio Ya Pamoja

Tumetaja kwa kifupi baadhi ya udangnyifu (au mvinyo unaolevya) ambao umepenya kidogo kidogo na kuingia ndani ya makanisa mengine. Lilikuwa ni jambo la kusikitisha pale shirikisho la Walutheri Duniani na Kanisa Katoliki,

| <b>AMRI KUMI ZA MUNGU</b><br><i>Kutoka 20: 2-17</i>  | <b>AMRI KUMI ZA MUNGU</b><br><i>Zilivyobadilishwa na binadamu<br/>(Toka kwenye katekismu ya Walutherani)</i> |
|--|--|
| <b>1. Usiwe na miungu mingine ila mimi.</b>  | <b>1. Ndimi Bwana Mungu wako usiabadu miungu wengine.</b>  |
| <b>2. Usiwe na miungu mingine ila mimi. Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukio, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.</b>  | <b>2. Usitaje bure jina la MUNGU wako.</b>   |
| <b>3. Usilitaje bure jina la Bwana, Mungu wako, maana Bwana hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.</b>   | <b>3. Shika kitakatifu siku ya Mungu.</b>  |
| <b>4. Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.</b> | <b>4. Waheshimu baba na mama upate miaka mingi na heri duniani</b>   |
| <b>5. Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako.</b>   | <b>5. Usiue</b>  |
| <b>6. Usiue.</b>   | <b>6. Usizini.</b>   |
| <b>7. Usizini.</b>   | <b>7. Usiibe.</b>  |
| <b>8. Usiibe.</b>  | <b>8. Usiseme uongo.</b>   |
| <b>9. Usimshuhudie jirani yako uongo.</b>  | <b>9. Usitamaman mwanamke/ mwanaume asie mke/mme wako</b>  |
| <b>10. Usitamani nyumba ya jirani yako, usitamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alichacho jirani yako.</b>   | <b>10. Usitamani mali za watu</b>  |




mnamo Octomba 31, 2000, walipatia sahihi azimio la pamoja kuhusu mafundisho yanayo angazia kuhesabiwa haki. Washiriki wengi katika kanisa la Kirutheri hata hawana habari ni yapi yaliyokusudiwa kwenye makubaliano haya, kwani uamuzi huu uliafikiwa na viongozi wenye uwezo katika makanisa hayo kufuatia mikutano ya wanachama bila ya watu kujua. Azimio hili pamoja husema, baadhi ya mambo mengine, ya kwamba sisi ni wenye dhambi, na wakati huohuo watakatifu. Lakini Biblia yasema kuwa bora tuwe tumeikubali haki ya Yesu, sisi sio wenye dhambi tena, bali sisi ni wenye haki (1 Yohana 1:9).

Isitoshe, kama tungalikuwa wenye dhambi saa zote, hakuna mtu ambaye angeokolewa. Kwani Biblia yasema kuwa hakuna kichafu kitakachoingia kwenye

Walutheri wanarudi Roma kuhusu swala hili muhimu? Ubatizo na komunyo, ambazo ni baadhi ya hizo waziitazo sakaramenti, ni mifano tu. Hatufai kutia chochote kati yetu na Kristo ili eti tujiokoe au tuipate haki. Ni pale tu tuendapo kwa Yesu Kristo kuzipeleka dhambi zetu ambapo hufanywa wenye haki.

### ***Kuwanyunyizia maji watoto wachanga***

Hilo "Azimio la Pamoja" kadhalika husema kuwa "ni kwa kusikia na kuamini ambapo mtu huhesabiwa haki kupitia ubatizo" Twajua ya kwamba ni kwa kuwanyunyizia watoto wachanga maji vichwani ambapo wao hupata tikiti ya kuingia kwenye makanisa ya Kikatoliki na ya Kilutheri. Lakini mtoto hawezi kuamini chochote akiwa peke yake. Pia, haifai watu wengine kuamini jambo kwa niaba yako. Biblia yasema Kuwa imani huja baada ya Neno la Mungu kuhubiriwa, na kuwa yeyote ambaye huamini na kubatizwa ataokolewa (Warumi 10: 17 na Mariko 16: 16). Ubatizo ni agano njema la dhamari kati ya Mungu na binadamu (1 Peter 3: 21), lakini mtoto mchanga hawezi kuelewa maana ya angano hilo. Itambidi mtu yeyote kwanza kuisikia Injili, kisha aamue ikiwa ataingia kwenye mkataka huu wa dhamili pamoja na Mungu au la. Isitoshe ubatizo wa Biblia ni kuzikwa ndani ya maji, ambapo mtu huyazika maisha ya zamani kwa mfano tu, na kufufuka katika maisha mapya pamoja na Yesu Kristo (Warumi 6: 3-6).



ufalme wa Mungu, naye Yesu alikuja kumwkoa binadamu toka dhambini, bali sio ndani ya dhambi (Ufunuo 21:27 na Mathayo 1:21).

### ***Haki Kupitia Kwenye Sakaramenti?***

"Azimio la Pamoja" pia husema kuwa waumini wanayo haki kabisa, kwa sababu Mungu huwasamehe kupitia kwenye neno na sakaramenti. Lakini, hatuwezi kuopokea msamaha na kuwa wenye haki kutokana na matendo yetu (yaani sakaramenti). Huu ni ukatoliki, na chanzo chake lilikuwa ni Baraza la Trent mnamo karne ya 16. Kwa nini

### ***Charta Oecumenica***

"Azimio La Pamoja" ni hati ya





mfuasi wa kweli wa Yesu huuchukua huo ukweli unotatanisha, na kumwomba Mungu amsaidie kuingiana na mapenzi ya Mungu katika nyanja zote.

Hiyo Charta Ecumenica pia itafanya kazi ili “kuyakuza masomo ya ki-ekumeni katika elimu ya Kikristo na katika mafunzo ya thologia na katika elimu ya juu”. Je, tutawezaje kuwakinga vijana wetu dhidi ya ushawishi huu mkuu wenye asili ya ki-ekumeni na kikatoliki?

Hilo “Azimio la Pamoja” kadhalika husema kuwa “ni kwa kusikia na kuamini ambapo mtu huhesabiwa haki kupitia ubatizo” Twajua ya kwamba ni kwa kuwanyunyizia watoto wachanga maji vichwani ambapo wao hupata tikiti ya kuingia kwenye makanisa ya Kikatoliki na ya Kilutheri. Lakini mtoto hawezi kuamini chochote akiwa peke yake. Pia, haifai watu wengine kuamini jambo kwa niaba yako. Biblia yasema Kuwa imani huja baada ya Neno la Mungu kuhubiriwa, na kuwa yeyote ambaye huamini na kubatizwa ataokolewa (Warumi 10: 17 na Mariko 16: 16). Ubatizo ni (Matendo 24:14), badala yetu kuwaachilia hawa wenye madaraka kutufunganisha na mpango wao wa kiekumeni na kikatoliki (soma zaidi kuhusu jambo hili kwenye kijitabu kiiwacho Charta Oecumenica).

kutatanisha, wala sio “asema Bwana “. Hivi majuzi, mashirika makubwa ya Kikatoliki na Kilutheri huko Uropa, nao ndio CEC (yaani Kongamano la Makanisa ya Uropa) na CCEE (Kongamano la Maaskofu wa Kikatoliki huko Uropa), wote walikusanyika pamoja ili kuiandaa hati ya pamoja iitwayo Charta Oecumenica . kwa mambo mengi, hati hii yafanana sana na ile mipango iliyofanywa na kanisa Katoliki pamoja na kundi la Wajesuti mnamo 1995. (yaani Toka kwenye Kongamano la Wajesuti 1995). Kumbukumbu za mkutano huu zaonyesha kuwa hao watajitahidi kuyaunganisha makanisa. Tena wanataka muungano huu uwe chini ya Kanisa Katoliki. Katika Charta Oecumenica, karibu umerudiwa mpango huo huo. Yasema hivi “Hadi pale tutakapolifikia lengo letu ambaloni Ushirikiano mkamilifu wa kanisa, twakusudia kufanya kazi pamoja katika mambo yale yasiyohusisha kuhitilafiana kwingi kwa imani ambako kwaweza kutu lazimu kutenda mambo katika hali ya kutengana “. ili kuyaafikia haya, wataingia katika MAJADILIANO pamoja makanisa yale mengine, ambapo hayo makanisa yatawajulisha kuhusu imani zao. Baadaye, watajaribu kuyakusanya yale wanayoyaamini kwa pamoja, na kuyaepuka yale yanayohushisha mabishano. Lakini

## CHARTA OECUMENICA

FOR THE  
CO-OPERATION  
OF CHURCHES IN  
EUROPE



Geneva /  
St. Gallen,  
July 1999



## MABINTI WA MAKAHBA

Hapa twona kuwa makanisa ya Kilutheri pamoja na makanisa mengine ambao hufanya makubaliano na kutia sahihi kwenye maazimio ya pamoja na kanisa Katoliki, na ambao huyashikilia mafundisho ya uongo kuhusu mambo muhimu, wamekuwa “Mabinti wa Makahaba”, kama Biblia inavyoeleza katika Ufunuo 17:5.

Twayapata maneno “Babeli” na “Mnara wa Babeli” katika kitabu cha Mwanzo, sura ya 10 na 11. Nimrod alikuwa ni mtawala, na ni chini ya utawala wake ambapo waliunjenga ule Mnara wa Babeli. Hapo mwanzo, “Babeli” ilikuwa na maana sawa na ile hali ya uasi dhidi ya mamlaka ya Mungu. Binadamu aliutwaa uongozi uliokuwa wa Mungu pekee. Kwa jinsi hii, “Babeli” akawa mama wa dini zote bandia, nayo dini yao ni hii iliyofundisha ya kwamba wangeokolewa kupitia kwa matendo yao wenyewe. Kulikuwa na utovu wa uungu, kujitwalia mamlaka na hali ya kuchanganyikiwa. Ndiposa twalinganisha “Babeli” na kuchanganyikiwa. Neno “Babeli” humanisha kuchanganyikiwa.

Mji wa Babeli, uliokuwepo miaka 600 kabla ya Kristo, pia ulikuwa na aina kama hizi za uasi na kuchanganyikiwa. “Utawala wa dunia” huu uliwadhulumu watu wa Mungu, nay Biblia huwaamuru watu wa nyakati hizo hivi:

**“Kimbieni kutoka kati ya Babeli, kila mtu na ajiokoe nafsi yake; msikatiliwe mbali katika uovu wake; maana ni wakati wa kisasi cha Bwana, atamlipa malipo. Tungependa kuuponya Babeli, Lakini haukuponyeka; Mwacheni, nasi twendeni zetu, Kila mtu hata nchi yake mwenyewe; Maana hukumu yake inafika hata mbinguni, Nayo imeinuliwa kufikilia mawinguni.”**

*(Yelemia 51:6.9)*

Hivyo basi Babuloni yaelezea vile kusanyiko bandia ambalo litaongoza wakati wa dunia hii. Kusanyiko hili bandia la Kibabuloni ndilo kanisa Katoliki, kwani linalo alama za kutabulisha sawa na zile ilizokuwa nazo Babuloni ya kale. Makanisa ya Kilutheri yamekuwa yakifanana na “Babuloni” hatua kwa hatua, hadi sasa wamekuwa sehemu ya “Babuloni” Biblia yaashiria kuwa mwanguko huo utakuwa mkuu, kwa kanisa Kikatoliki na pia kwa Walutheri... Hali kadhalika kwa wale wote wafuatao njia hiyo hiyo... Yatadhihirishwa hivi karibuni.

Japokuwa makanisa ya kibabeli yamekumbwa na giza la kiroho na pia kutengana na Mungu, sehemu kubwa y a wafuasi wa Kristo wapatikana mumo humo. Wengi wao bado hawajayafumbua macho



yao ili kuufahamu ukweli huu wa nyakati hizi. Kunao wachache wasioridhika, ambao wanatumaini kuona mwangaza zaidi. Hawa wanaitafuta sana sura ya Kristo kwenye makanisa wanayohudhuria, bila mafanikio. Huku makanisa haya yakiendelea kutanga mbali na ukweli, na kujifunganisha na ulimwengu, polepole, hatua kwa hatua, tofauti kati ya vikundi hivi viwili itaendelea kudhihirika. Hatimaye kutakuwa na utengo kamili. Wakati unakaribia ambapo wao wampendao Mungu zaidi ya mengine yote hawataweza tena kushiriki pamoja na wale walio na...

**“wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake; hao nao ujiepushe nao.” (2 Ti. 3:5)**

Shauri la Biblia kwetu, sisi katika nyakati hizi za mwisho ni wazi kabisa:

**“...TOKENI KWAKE, ENYI WATU WANGU,...”**  
*Ufunuo 18:4*

## UMOJA NDANI YA KRISTO

Harakati za ekumeni hujaribu, kupitia kwenye maafikiano na utawala wa wengi, kuyafanya makubaliano kuhusu maswala kadhaa ambayo hayahusishi mabishano mengi, na kuyaacha yale ambayo yanaleta ubishi. Hata hivyo, Biblia yasema kwamba neno la Mungu ndilo linalofaa kutuonyesha njia. Ni kwa namna hiyo tu ambapo tutaufikia ule wa kweli.

Biblia hupendekeza umoja, lakini umoja huu ni lazima uwe umejegwa juu ya msingi dhabiti wa Biblia na sharti kuwe na umoja ndani ya Kristo.

Yesu huuelezea namna hii:

**“...ili wawe wamekamilika katika umoja; kama wewe, Baba, ulivyo**

**ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu...” (Yohana 17:21-23)**

Watoto wote wa Mungu watasimama pamoja ili kuafikia umoja ndani na pamoja na Kristo. Umoja utafika kulingana na kile kipimo alichokiweka Mungu, ambavyo mara nyingi haviwi juu ya msingi wa “asema Bwana”.

## TOKENI BABELI

Biblia huelezea hali ya mambo yatakavyokuwa nyakati za mwisho hivi:

**“na mdalasini, na iliki, na uvumba, na marhamu, na ubani, na mvinyo, na mafuta ya mzeituni, na unga mzuri, na ngano, na ng’ombe, na kondoo, na farasi, na magari, na miili na roho za wanadamu.” (Ufunuo 18:3).**

Hii ni hali ya kutatanisha, hata hivyo kunayo nuru gizani. Mungu angali ana watu wake huko “ Babuloni, ” nao wataipokea changamoto kubwa hasa nyakati hizi za mwisho. Kundi fulani litaibuka, ambalo lafananishwa na malaika. Nao litazitangaza dhambi za “ babeli ” kwa sauti kuu. Ujumbe wenyewe ni:

**“Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake.” (Ufunuo 18:4).**

Tangazo hili, pamoja na ule “ ujumbe wa malaika wa tatu, ” ndilo onyo la mwisho kwa wanadamu. Iwapo wewe hujichukulia kwa sehemu ya watu wa Mungu, yakupasa ulikubali onyo hili, ukajiepushe na ushawishi wa e kumeni.

Hatimaye hatautazama ule ujumbe wa mwisho ambao wanuiwa kutangazwa sasa hivi, yaani muda mfupi kabla ya kuisha kwa wakati tuliopewa wa rehema na kabla ya kurudi kwa Yesu.

# Ujumbe Wa Tatu

***“Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo. Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake. Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu.”***

*Ufunuo 14:9-12*

## MHURI WA MUNGU AU ALAMA YA

“Alama ya mnyama “ ama “ alama ya Mungu “ ndilo chaguo litakalokuwepo nyakati za mwisho. Lahusu uamuzi kati ya kumtii Mungu au binadamu. Mungu ametukabidhi muhuri au alama yake ndani ya ile amri yake inayohusu siku ya kustarehe. Muhuri hushirikisha jina la mpaji wa sheria, madaraka yake na hatimaye milki yake, amri inayohusu siku ya kustarehe yasema hivi:

**“Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.” (Kutoka 20:8-11).**

Hapa yasema kuwa jina la mpaji wa sheria ni “ Bwana “ na madaraka ya huyu mpaji wa sheria ni yule “ aliyeeumba “ (yaani muubaji ) nayo milki ya utawala wake ni “ mbingu na nchi na bahari, na vyote vilivyomo.” Kanisa

Katoliki limekiondoa kifungu hiki cha maneno kutoka kwenye amri kwa majibu wa katekismus yaani, kifungu kinachodhihirisha kuwa Mungu ndiye mtunzi wa sheria kimeondolewa.

Wakishafanya hivyo, wanajitwalia uhuru kwa kujifanya watunzi wa sheria wenyewe, kisha wakazibadili amri na kuzifanya kama tunavyoona kwenye katekismus yao.

Nabii Daniel aliwahi kuandika kuhusu kuibuka kwa dini fulani (Daniel 7:25). Japokuwa upapa umeshautimiza unabii huu tayari kwa kule kuzibadili amri kumi za Mungu kwa mjibu wa katekismus, hata hivyo amri za Mungu zingali halali. Yesu asema hivi:

**“Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie.”**  
*(Mathayo 5:17-18).*

Kanisa katoliki limeondoa sio tu sehemu kubwa ya lile fungu linalozungumziasiku ya pumziko katika amri, bali pia maneno yanayotumuru kumwabudu Mungu katika siku ya saba kulingana na Biblia. Wala sio jumapili, ambayo Biblia huitaja kuwa siku ya kwanza juma. Kwa bahati

mbaya, kanisa la Kilutheri l i m e k u w a likizifuata nyayo za kanisa katoliki.

Hivyo basi waweza tu kukipata kifungu kifupicha maneno kifuatacho ndani ya katekismusu ya Lutheri "itakase siku ya pumziko". Hapa haujajurishwa ni gani siku ya pumziko bandia, aliyoianzisha b i n a d a m u , wala sio iku ya kustarehe ya Biblia.

M a g e u z i siku ya pumziko toka sabato hadi jumapili yalifanyika zaidi ya miaka elfu kabla ya waleashujaa au matengenezo. Leo hii, wachache tu wafahamu kuhusu undanganyifu huu, na wengi hutunza jumapili kama siku ya pumziko pasipo nia mbaya, huku wakiamini kuwa hiyo ndiyo siku ya starehe kulingana na Biblia. Lakini hapa ndipo makuhani na wachungaji wamewahadaa watu, huku wakikataa kulihubiri Neno kwa uzazi na usafi jinsi lilivyo kwenye maandiko matakatifu.

### SABATO NI SIKU GANI?

"Lakini siku ya saba ni gani kulingana na Biblia?" huenda utauliza. Kuambatana na kifo cha Yesu, na mazishi, na kufufuka kwake, Biblia huitaja siku aliyofariki Yesu kuwa "siku maandalizi" au "siku inayoitangulia sabato". Pia hujulikana na wengi kama Ijumaa njema, siku ambayo Yesu alifufuka toka kabulini huitwa siku ya kwanza ya Juma, yaani Jumapili kwa lugha ya kisasa. Siku iliyokatikati ya hizi mbili huitwa "sabato" "siku ya saba" yani Jumamosi. Yesu, aliye Bwana wa sabato, alipumzika kaburini mnamo Jumamosi, kisha akafufuka kuikabili siku mpya ya kazi, yaani Jumapili kwa hivyo jumapili kulingana na Biblia ndiyo siku ya mwanzo wa zile siku sita za kazi katika juma. Katika Biblia, siku

huanzia machweo hadi machweo (Mwanzo 1: 14-19, Walawii 23:23, Nehemia 13:16-21, Luka 23: 54-56).

Hivyo basi siku ya saba kulingana na Biblia, yaani sabato, huanzia machweo Ijumaa na kumalizika machweo jumamosi.


Leo hii, kanisa katoliki pamoja na baadhi yamakanisa ya Kiprotestanti huita jumapili "siku ya Bwana" (15,58:13) kwa hivyo "siku ya Bwana" siyo jumapili, bali ni sabato.



### DIES DOMINI

Aliyekuwa papa Yohana wa Pili katika barua yake ya uchungaji, "Dies Domini" ya Mei 1998 alitambua ya kwamba sabato ndio siku asili ya pumziko ya Mungu, lakini asema, bila ya kuona haya, ya kuwa "Wakristo, ambao wameitwa ili kutangaza uhuru uliyoshindaniwa na damu ya Kristo, walihisi kuwa wanayo mamlaka ya kuihamisha maana ya sabato hadi kwenye siku ya ufufuo" pia huyo Papa anazungumzia "utajiri wa kiroho na wa kiuchungaji uliomo ndani ya jumapili, kama ilivyokabidhiwa kwetu na utamaduni." pia Papa akasema kuwa Walihisi kuwa wanayo mamlaka ya kuyatekeleza m a b a d i l i k o haya, na pia anakubali ya kuwa kuwepo kwa jumapili kama siku ya m a p u m z i k o kumetokana na utamaduni.

"Jumapili ni ya wakatoliki, na pendekezo lao eti kuwa





## BAADHI YA HOJA MUHIMU

# **Akitoka ndani ya bahari – Ufunuo 13:1 Bahari/ maji = watu, umati, mataifa – Ufunuo 17:15.**

Utawala wa upapa uliibuka magharibi mwa bara Uropa , mahali ambapo mna watu wengi sana.

# **Hupokea nguvu zake, kiti chake na mamlaka kutoka kwa joka – Ufunuo 13:2.**

# **Huwa ni uwezo mkuu duniani unaopokea ibada – Ufunuo 13:3-8.**

**Katoliki humanisha dunia nzima. “Ndilo kanisa lenye nguvu na ushawishi mkuu duniani.”**

# **Hupokea jeraha la mauti japo hupona – Ufunuo 13:3.**

Mnamo mwaka wa 1798 Generali Barthier alimteka nyara Papa hadi Ufaransa alikofia ugenini. Mnamo Februari 11, 1929 Dikteta Benito Mussolini Na Papa Pius XII walitia saini mkataba wa uliounda ‘uongozi wa Vatican’ – kanisa huru katika jimbo huru.

# **Amevaa zambarau na nyekundu iliyopabwa kwa rangi ya mawe ya dhahabu na lulu. Ufunuo 17:4.**

Hii ndio rangi ya mavazi ya makadinali na maaskofu wa kanisa Katoliki.

# **Ana hatia ya kukufuru. Ufunuo 13:1,5,6**

“Sisi (Papa) hapa ulimwenguni tunashikilia nafasi ya Mwenyezi Mungu” Papa Leo XII

“Kasi kwa hakika na ukweli husamehe dhambi kwa fadhira na nguvu alizopewa na Kristo.” Joseph Deharbes, S. J. Katekismus kamilifu ya dini ya Katoliki ukurasa 279.

# **Alitawala kwa miaka 1260 – Ufunuo 13:5-7, Daniel 7:25. 538 BK -1798 BK (FEB 10)**

Hesabu za kinabii- Ezekiel 4:6 – Siku moja kwa mwaka na Kibibilia siku 30 kwa mwezi.

# **Huwadhoofisha watakatifu wa Mungu – Ufunuo 17:6 akalewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yesu.**

**Kwa zaidi ya watu milioni 80 waliteswa na kuuawa wakati wa kipindi cha mateso ya kipapa.**

# **Rumi inafahamika sana kwa kuwa imejengwa kwenye vilima saba. Ufunuo 17:9 ... vile vichwa saba vinawakilisha milima saba. “ la citta dei sette colli” .**

„La citta dei sette colli“ – mji wa milima saba.

# **Vadovauja vienas viršiausią žmonių – Ufunuo 13:18.**

# **Anayo na nambari ya siri 666 – Ufunuo 13:18. Mada rasmi ya kumrejelea Papa ni – “Vicarius Filii Dei” = 666 (Msaidizi wa Mwana Wa Mungu).**

itakaswe laweza tu kutetewa kuambatana na imani ya kikatoliki.” (The Catholic Press, Sydney, Australia, August 1900).

Sasa ni dhahiri kuwa zile ishara zote zilizotolewa na Biblia za kumtambua Mpinga Kristo, iloisemekana pia vivyo hivyo katika lile azimio liitwalo “Augsburg Confession of Belief.” Ukurasa 5:39

Tumeona jinsi kanisa katoliki lililouondoa ule mhuri wa Mungu au alama yake toka kwenye amri zake, kama isemavyo katika katekismus yao, na ya kwamba wao huendelea kusema, kwenye jumbe zao mbali mbali, ya kuwa jumapili ndiyo alama yao ya mamlaka, na kuwa wengi wao huyatambua mamlaka ya kanisa lao hili kwa kule kuitakasa Jumapili (H.F. Thomas, chancellor of Cardinal Gibbons, and the Donay Catechism, p. 59).

## KOMUNYO NA UTUNZAJI WA JUMAPILI

Katika ile bana yake ya uchungaji iitwayo Dies Domin, aliyekuwa Papa Yohana wa pili aliwahimiza makasisi kupeana komunyo ya kikatoliki kila Jumapili. Maana yake ni kuwa aliwaambia watu wazitangulize tamaduni mbili zisizo za kibibilia kwa pamoja, nazo twaweza kuona waziwazi jinsi mambo yanavyoendelea kukomaa, kama vile aliyekuwa Papa Yohana Paulo wa Pili alivyosema katika barua yake iliyochapishwa mnamo Mei 28, 1998, ya kuwa mtu yeyote atakaekataa kuzitunza sera za kikatoliki, “ataadhibiwa kama mwasi” maneno yaha ni sawa na upepo ule uvumao toka enzi zile za kale. Lakini usiwe na hofu yeyote anayeongozwa na kristo, anaye mmoja aliye mwenye nguvu zaidi kwa upande wake, naye atawapa watoto wake nguvu tosha za kushinda, japo watakabiliana na vitisho pamoja na mateso.

## HESABU YA MNYAMA

Katika kijitabu kiitwacho, “Watch out for the power Elite and the Global Union!” twazipata alama 16 za kumtabulisha “mnyama.” Alama zote hizi zaingiana na kanisa katoliki, hali kadhalika ile hesabu ya mnyama, yaani 666. Biblia yasema kuwa hii ni NAMBARI YA MTU FULANI, wala sio namba ya tarakimu fulani zenye mafumbo. Wale

# "VICARIUS FILII DEI"

|         |        |           |
|---------|--------|-----------|
| V = 5   | F = 0  | D = 500   |
| I = 1   | I = 1  | E = 0     |
| C = 100 | L = 50 | I = 1     |
| A = 0   | I = 1  | 501       |
| R = 0   | I = 1  |           |
| I = 1   |        | 53        |
| U = 5   |        | JUMLA     |
| S = 0   |        | ZOTE NI = |
|         |        | 666       |
|         |        | 112       |



## KWENEY KIPAJI AU MKONO

Biblia yasema kuwa alama ya mnyama itapokelewa kwenye kipaji au mkono. Yasema hivi:

**"Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake."** (Ufunuo 13:16-17)

wanaopendekeza kuwa alama ya mnyama ni mfumo watarakimu hizo wanawapotosha watu. Hayo hayana uhusiano wowote na alama ya mnyama. Hata hivyo, yawezekana kuwa mfumo huo unaohusisha nguvu za umeme huenda ukatumiwa kwa kuwatabulisha watu, na kuhakikisha kuwa wale wanaokataa kuipokea alama hiyo ya mnyama hataweza kununua wala kuuza.

Lakini hebu tuirejeele namba ya mnyama Biblia yasema kuwa hiini namba ya mtu fulani. Naye ni nani?

Papa wote huwa na jina fulani la heshima, nalo ndilo VICARIUS FILII DEI, maana yake "mwakilishi wa mwana Mungu" hapa duniani. (soma Our Sunday Visitor, Catholic Weekly, Bureau of Investigation, Huntington, India 18th April 1915). Herufi za Kilatini huwa na maana fulani ya tarakimu, hivyo basi ukizilinganisha herufi hizi na hizo numerali, utapata 666. (V na U = 5, I = 1, C = 100, A = 0, R = 0, S = 0, L = 50, D = 500, E = 0). Jumla ni 666.

"Hesabu ya mnyama," "alama ya mnyama" na "sanamu ya mnyama," hizi ni alama tatu tu miongoni mwa zingine nyingi zitumikazo kutambua huyo " mnyama. " Alama zote lazima ziingiano utawala fulani, nazo huingiana na utawala wa Upapa. Luther na mashujaa wengine wa matengenezo hawakukosa pale waliposema kuwa "Papa anazo alama zinazo mtambulisha mpinga Kristo".

Hapa Biblia yajielezea yenyewe, huku ikisema kuwa kipaji chahusiana na kichwa pamoja na mawazo, nao mkono wahusiana na matendo (soma kumbukumbu 6:6-9 na kutoka 13: 8-10)

Wakati wa alama ya mnyama ukishawadia, wale ambao watakuwa wameshaambiwa na kuelewa haya yote, lakini wakachagua mawazoni, mwao kuitunza amri ya upapa ya jumapili, wataipokea vipajini mwao. Wale watakaoipokea alama mikononi mwao, hudhihirisha kwa mikono na matendo chaguo lao ni lipi. Hufanya kazi siku ya sabato ya Bwana, huku wakiipumzisha mikono yao siku ya sabato bandia, wote wawili hawa huipokea " alama ya mnyama".

Kwa kifupi, kuipokea alama ya mnyama maana yake ni kwamba mtu huyo amefanta uamuzi sawa na ule alioufanya yule MNYAMA, na atazitetea hisia hizo hizo japo zapingana na neno la Mungu.

Japokuwa watu wengi wanaipokea ishara hii ya utiifu kwa utawala wa kidunia na njia hiyo hupokea " alama ya mnyama " kipo kikundi idogo cha watu waliochagua kumtumikia Mungu, na kumkubali awe mtawala wao, hivyo basi wameupokea " mhuri wa Mungu. "

Kwa wale watakapoikea "alama ya mnyama," onyo hii latolewa toka mbinguni:

**“Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo.”**  
(Ufunuo 14:9-10)

“Lakini hakuna atakayeangukiwa na ghadhabu ya Mungu hadi pale ukweli utakapokatiliwa baada ya kusukumia kwenye mawazo dhamiri yake. Wapo wengi ambao bado hawajapata nafasi ya kuusikiliza ukweli huu wa kipekee kuhusu nyakati hizi. Jukumu la kuitii amri ya nne haijawahi kufikishwa kwao katika ile nuru kufikishwa kwao katika ile nuru ya kweli. Yeye asomaye kila moyo, achunguzaye nia zote, hatamwachilia yeyote anayetamani kuujua ukweli kudanganywa kuhusu pambano hili. Amri hii hawapasi kusukumia watiu kwa njia ya upofu. Kila mmoja atapata nuru tosha ili aweze kufanya uamuzi baada ya kutafakali kwa makini” ( The Great Controversy; p, 605 ) Kwa bahati mbaya, watu wengi zaidi watahindiwa pale wakapobanwa na serikali hadi waipokee alama ya mnyama, huku wakiogopa kupoteza kazi zao au kuishi bila chakula na nguo. Lakini mfuasi halisi wa Kristo atakuwa na hakikisho ya kuwa Mungu atamuwezesha kupitia kwenye hatari wakati itakapowadia.

### UTACHAGUA UTAWALA GANI?

Katika kijitabu hiki, umepewa nafasi ya kuchagua ni mtawala gani utakaomfuata Yesu aliyesimamisha sabato (Jumamosi ) au upapa, ambao hupendekeza kuitakaza jumapili, kuhusu jambo hili, tutatoa maelezo zaidi. Yesu alihusika kwenye uumbaji Biblia yasema “vitu vyote viliumbwa na yeje” (Yohana 1:1-3, 14). Alishiriki

katika kuisimamisha sabato, nayo Biblia husema ya kwamba Yesu ndiye Bwana wa sabato (Mariko 2:28 ). Kwa hivyo, kama angalihitajika mtu wa kuibadilisha sabato, bila shaka angalikuwa ni Yesu. Lakini je, waweza kulipata neno hata moja kutoka kinywani mwa Yesu linalotushauri kuacha kuitunza sabato na kwanza kuitunza Jumapili kama siku ya kustarehe? Tulishasoma hapo awali ya kwamba hakuna herufi hata moja itakayotolewa kwenye sheria. Biblia pia husema kuwa...

**“Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele.”**  
(Waebrania 13:8)

Hapa twaambiwa kuwa amri za Mungu zingali za simama, ikiwemo amri za sabato.

Kwa hivyo swali ni hili; utamchagua mtawala gani ; wale wanaoifuata amri ya kibinadamu pamoja na jumapili kama siku ya pumziko, au Mungu na siku yake ya pumziko ambayo ni sabato (yaani jumamosi).

Biblia yasema kuwa jibu lako kwa swali hili litakuwa ndilo jaribio la mwisho nyakati za mwisho je, utamwabudu Mungu na kumtii kwa kuitunza sabato? (Ufunuo 13:15-17 na 14:9-12).

Kila mtu atafanya uamuzi baada ya kufafanuliwa mambo haya. Kijitabu hiki chanuia kukusaidia kufanya uamuzi huu, lakini waweza kusoma zaidi kuhusu swala hili kwenye kitabu kiiwacho “Vita Kuu” au kikatataji kiiwacho “Uhuru Hatarini.” Hivyo basi sabato itakuwa ndilo jaribio kuu la uaminifu, kwani pambano lenyewe lahusu swala la ukweli na ibada. Watu wakishatiwa kwenye jaribio hilo la mwisho. Msitari utachorwa kati ya wale wamchao Mungu na wale hapana. Kuisherehekea sabato bandia kulinganana sheria za nchi, lakini kinyume na amri ya nne litakuwa ni tangazo la utiifu kwa utawala unaopingana na Mungu ni tangazo la utiifu kwa muumbaji. Huku kundi moja likiikubali alama ya utiifu kwa tawala za dunia, kundi lingine huchagua alama ya utiifu kwa utawala wa Mungu, hivyo basi wataupokea “mhuri wa Mungu”.



## MHURI WA MUNGU KIPAJINI MWAKO


Ijapokuwa alama inayoonekana ya Mungu imo ndani ya ile amri yake inayohusu siku ya pumziko, japo Mungu asema kuwa sabato itakuwa ni ishara kati yake na watu wake (Ezekieli 20: 12, 20) twaelewa pia ya kwamba mhuri watakaoupokea watoto wa Mungu vipajini mwao muda tu kabla ya mwisho wa ule msukosuko w a dunia, utakuwa ni mhuri wa aina ya kipekee. Mhuri huu utatiwa juuya wa aminifu watakaonusurika na kuibuka washindi katika vita dhidi ya “alama ya mnyama.”

“Mhuri wa Mungu” ni ishara ya kwamba Mungu hupendekezwa na watoto wake. Biblia yasema kuwa wale wanaotubu na kumwamini kristo

wameahidiwa Roho mtakatifu kama mhuri. Mwamini anaye Roho mtakatifu kama mhuri maishani mwake bora tu awe anaishi karibu na kristo na kuyatenda mapenzi yake. (Waefeso 1:13 na Matendo 5: 32).

Lakini sasa tutaangalia kule kutiwa mhuri kutakaofanywa na malaika wa Mungu muda kidogo kabla ya kurudi kwa Yesu. Biblia yasema kuwa malaika wa Mungu atautia “mhuri wa Mungu” vipajini mwa wale wanaolia na kuomboleza kwa ajili ya machukizo yanayopatikana na kutendwa miongoni mwa wale wanaojidai kuwa viongozi wa kiroho wa watu wa Mungu. “mhuri wa Mungu” ukiwepo kipajini ni ishara ambayo ni malaika pekee (wala si binadamu) wanaoweza kuiona (Ezekiel 9: 4) “mhuri wa Mungu” ukiwepo kipajini humaanisha ile hali ya kutosheka ndani ya ukweli, kimawazona pia kiroho hivi kwamba watoto wa Mungu hawawezi kutikisika (ufunuo 14:1-6)

Wale ambao hawajitegemei, bali hujinyenyekeza mbele za Mungu, ambao kwa nguvu za Roho mtakatifu huishi kulingana na mapenzi ya Mungu, huwa wameshaipokea chapa ya mbinguni huku wakijiandaa kuupokea “mhuri wa Mungu” au chapa ya kukubaliki, watapewa wale tu walio na Roho wa Mungu, nao



kwa jinsi hiiwatatiwa nguvu Rohoni hivi kwamba hawataweza kutikisika. Hakuna atakayewadhuru wakati wa yale mapigo, nao wameshajiandaa kuwa na kristo wakati ajapo kuwachukua wafuasi wake.

Kisha Biblia hutufunulia ya kwamba hiyo “alama ya mnyama” itaonekana kabla ya kumalizika kwa muda wa rehema, na pia kabla ya kurudi kwa Yesu (Ufunuo 13:11-6) Twasoma kuhusu wale ambao...

**“Tena nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo iliyochangamana na moto, na wale wenye kushinda, watokao” (Ufunuo15:2).**

Yohana pia aliweza kuwaona hao walioibuka washindi dhidi ya alama ya mnyama; huku wakiwa wamesimama mbele ya kiti cha enzi cha Yesu kilichoko mbinguni (Ufunuo 4:2 na 7:9) WALIIBUKA WASHINDI hii yamaanisha kuwa hapo mbeleni walikuwa katika pambano fulani hivyo basi wateule watakaokuwa bado hai arudipo Yesu watakuwa wamesharipitia lile jaribio kuu linalohusu “alama ya mnyama.”

“Mhuri wa Mungu” au “alama ya mnyama” hii ndilo litakalokuwajaribio kuu litakaloamua mwisho wa kila mmoja wetu. Huu ndio

mtihani ambao itawabidi masalio wa Mungu kuupita kabla yao kutiwa ule mhuri. Wote watakaodhihirisha utiifu wao kwa kuitunza sheria ya Mungu, na watakaokataa kuipokea ile sabato bandia (yaani jumapili watakuwa wamejitikia chini ya bendera ya Mungu, na wataipokea “ mhuri wa Mungu aliye hai. “Wale watakaoionea haya ile kweli itakayo kwa Mungu, na watakao ikubali ile sabato ya Jumapili, wataipokea ishara ya mnyama.

Sasa ndio wakati wa kujiandaa. “ mhuri wa Mungu “ kamwe hautatiwa kwenye kipaji cha mke au mume aliye mchafu kamwe hautatiwa kipajini mwa mume au mke aliye na tamaa, au aupendaye ulimwengu. Wala hautatiwa vipajini mwa waume au wake walio na ndimi za uongo au roho zenye hila. Wote watakaoupokea muhuri huo nisharti wawe bila kosa mbele za Mungu kama vile watu ambao wazo lao kuu ni mbingu.

### HARAKATI ZA KUIPENDEZA JUMAPILI ZIMEANZA

Kunazo harakati za kuipendekeza jumapili zinazoendelea duniani kote. Papa Francis mjasus atatia nguvu pumziko la siku ya Jumapili kama siku ya kustarehe vikundi vikuu vya kidini, kama vile “The Christian Coalition,” vyatambia ya kwamba ni lazima tuzirudie zile


amri kumi za Mungu. Katika muungano wa Uropa (EU), Waprotestanti na Wakatoliki wanajaribu kuyatafuta maswala ambayo wote wanaweza kukubaliana, moja wapo likiwa ni kuichukulia jumapili kama siku ya pumziko. Huko Uropa muungano wa madhehebu, yaani CEC, wanania kuyaunganisha makanisa yote pamoja kulingana na mpangilio wa kikatoliki, na jumapili itatiliwa mkazo kama siku ya pumziko kwa watu wote, wakati Herald V alipowekwa taji kama mfalme wa Norway, alitaka shereheya kumbariki ifanyike mnamo

siku ya jumapili ili siku hiyo ya jumapili itiliwe mkazo kama siku ya kupumzika. Makasisi na makuhani wanatamani sherehe za jmapili zifufuliwe. Wengine wanataka harakati zinazohusu watu wote wa kuitetea siku hii iwe ya pumziko, huku wengine wakipendekeza adhabu kali kwa wale watakao haribu amani ya siku hiyo takatifu.

Twaona pia jinsi makasisi na wachungaji wanavyojuunga vya wafanya kazi, mashirika yakulinda mazingira, hali kadhalika matawa mbalimbali ya biashara na viwanda, ili waweze kuilinda jumapili na kuifanya kuwa siku tofauti na zinginezo katika juma. Nia zao huenda ni nzuri, kwani ni jambo la busara kutoka kuifanya siku ya pumziko kuwa ni ya kuridhisha. Kwa kweli yafaa tustarehe, tupumzike na tuweze kuburudika kiroho na pia kimwili. Lakini kama ingelihatijika wakristo kuipendekeza siku ya pumziko, yafaa iwe ni ile siku ambayo muumbaji ameitakasa na kuibariki, yaani sabato, siku ya saba ya jumaa kulingana na Biblia. Isitoshe haifai mtu yeyote alazimishwe kuitunza siku ya pumziko ambayo serikali imeamua. Kuitakaza siku ya pumziko ni kwa hiari, wala si lazima. Lakini Biblia yasema kuwa uhuru wa kuabudu utadharauliwa katika swala hili. Hata sasa tayari twayaona matayarisho ya vikwazo kama hivyo vya kidini.

### ALAMA YA MNYAMA ITAFIKA HIVI KARIBUNI

Jaribio kuhusu “alamaya mnyama” litafika pale jumapili itakapo simamishwa kimabavu, na kwa amri, kama siku ya kupumzika, jambo ambalo laweza kufanyika hivi karibuni. Hata hivyo, kwa vile sasa twajua kuhusu undaganyifu uliofanywa dhidi ya siku ya pumziko, yatupasa pia tufanye uamuzi leo (Yakobo 4:17). Ni jambo la muhimu kwetu sisi leo kujitia kabisa kwenye upande wa Yesu kuhusu swala



hili, ili Roho mtakatifu awe mwenye kuutia nguvu tunapokabiliana na majaribu yaliyo mbele yetu ambayo yahitaji uamuzi.

### MASALIO WATAVUMILIA WATAZITUNZA AMRI ZA MUNGU NA MAFUNDISHO YA YESU

Biblia yawaelezea wale ambao hawataikubali sabato bandia ya kibinadamu jinsi hii:

**“Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu.”**  
(Ufunuo 14:12).

Kwa hivyo, hebu na tuzijue amri za Mungu pamoja na yale yote aliyoyaamini Yesu.

Biblia yadhahirisha wazi kuwa litakuwepo pambano kali la kiroho mnamo siku za mwisho kabla ya kurudi kwa Yesu wale ambao hawataikubali alama ya mnyama watafinyiliwa toka pande zote. Yasemekana ya kwamba hawataweza kununua wala kuuza, na kuwa amri itatolewa ili wauawe (Ufunuo 13:15-16). Dunia yote itaustaajabia upapa ( yaani mnyama ) na hata kumfuata, lakini masalio wa Mungu walio waaminifu hawatawezwa na mvuto huo, Biblia yasema kuwa hawa hawakujinajisi na wanawake (yaani makanisa, 2 Wakoritho 11:2), kwani wao ni kama bikira. Kwa kifupi, hawaupokei “mvinyo wa Babuloni unaolevya,” lakini hutangaza, kwa sauti safi, ule “ujumbe wa malaika watatu,” na pia huionyesha tabia ya Mungu maishani mwao. Hawauachilii ubinafsi wao uongoze, bali huifuata njia ya Mungu huku wakiongozwa na Roho mtakatifu, kuhusu hawa yasemekana...

**“Hawa ndio wasiotiwa unajisi pamoja na wanawake, kwa maana ni bikira. Hawa ndio wamfuatao Mwana-Kondoo kila aendako. Hawa wamenunuliwa katika wanadamu, malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo.”**  
(Ufunuo 14:1-5)

Kwa hivyo, hebu na tuzijue amri za

Mungu pamoja na yale yote aliyoyaamini Yesu.

Biblia yadhahirisha wazi kuwa litakuwepo pambano kali la kiroho mnamo siku za mwisho kabla ya kurudi kwa Yesu wale ambao hawataikubali alama ya mnyama watafinyiliwa toka pande zote. Yasemekana ya kwamba hawataweza kununua wala kuuza, na kuwa amri itatolewa ili wauawe (Ufunuo 13:15-16). Dunia yote itaustaajabia upapa ( yaani mnyama ) na hata kumfuata, lakini masalio wa Mungu walio waaminifu hawatawezwa na mvuto huo, Biblia yasema kuwa hawa hawakujinajisi na wanawake (yaani makanisa, 2 Wakoritho 11:2), kwani wao ni kama bikira. Kwa kifupi, hawaupokei “mvinyo wa Babuloni unaolevya,” lakini hutangaza, kwa sauti safi, ule “ujumbe wa malaika watatu,” na pia huionyesha tabia ya Mungu maishani mwao. Hawauachilii ubinafsi wao uongoze, bali huifuata njia ya Mungu huku wakiongozwa na Roho mtakatifu, kuhusu hawa yasemekana.

### SANAMU YA MNYAMA

Kwa vile Upapa unaingiana na zile alama za kumtambulisha “ mnyama ” kulingana na Biblia, basi “ sanamu ya mnyama ” sharti iwe ni nakala ya mfumo huu.

Maana yake “ sanamu ya mnyama ” ni Uprotestanti ulioasi ambao hutokea wakati makanisa ya Kiprotestanti yanapoanza juhudi za kuishawishi serikali kuwalazimisha watu waufuate mtindo wao wa ibanda.

Huko Uropa, nchi nyingi zinalo kanisa fulani linalopendekezwa na serikali. Serikali na kanisa hufanya kazi pamoja. Kanisa hupata msaada kutoka kwa serikari ili kute keleze majukumu yake. Huu ni sawa na mfumo wa kikatoliki. Katika Enzi za katikati za Giza, tulikuwa mfano halisi jinsi kanisa katoliki lilivyotumia nguvu zake na kuwatesa watu wa imani zingine. Biblia yasema kuwa ukatili kama huo utarudishwa mnamo siku za mwisho (Ufunuo 13:11-18). Kwa vile katiba ya Marekani haina nafasi ya kanisa la kiserikali, ni vigumu kudhania ya kuwa hapo ndipo mfano wa ile serikali



ya upapa itakaposimamishwa, lakini Biblia yadhahirisha kuwa hivi ndivyo mambo yatakavyotendeka. Wataitumia serikali ili kujisukumia sheria zao za kidini, hasa sheria zinazohusu utakasaji wa jumapili.

Lakini huenda utasema kuwa Marekani ni nchi ya uhuru wa kuabudu. Kweli, Biblia huielezea pia kama mwana kondoo aliyepembe mbili lakini anenaye kama joka. Mwanzoni mwa historia yake, Marekani ilionekana kuwa nchi inayoutetea uhuru wa dini. Pembe za mwana kondoo husimamia ujana, bila hatia na upole ambazo zilikuwa ni sifa za Marekani wakati ambapo nchi hiyo ilianza kukua mnamo karne ya 18. Uprotestanti na Ujamhuri zilikuwa ndizo sera zilizokuwa msingi wa serikali. Uhuru wa dini ulidumishwa, hivi kwamba kila mmoja alikuwa huru kumwabudu Mungu kulingana na dhamira zake hata hivyo Biblia yaonyesha kuwa mtindo huu utabadilika katika nchi hiyo hadi mwishowe, itanena kama joka. Kwa kawaida, taifa hunena kupitia kwa bunge lake.

Wengi sasa wametambua kuwa bunge la Congress limeshaanza kupitisha sheria za kidini, kama vile HR 2431, sheria hii huipatia afisi mpya iliyoteuliwa mamlaka ya kuvichunguza vikundi vya kidini duniani kote. Wale ambao wanayatekeleza mateso ya kidini wataadhibiwa. Afisi hii itamua maana ya mateso ya kidini. Kwa mfano je, kijitabu

chaweza kusemekana kuwa kinawatesa wakatoliki.

Katiba ya marekani yasema kuwa kamwe hatutapitishwa sheria zinazohusu dini. Yasema hivi, "Bunge kamwe halitatengeneza sheria kuhusu utanguluzi wa dini, wala kuuzuia uhuru wa kuyatekeleza majukumu ya kidini." Ni kwa kulidharau hakikisho hili la uhuru ambapo utawala wa serikali utawasukumia watu sheria hizo za kidini. Utaratibu huu tayari umeanza, na mengine mengi yaja. Ndiyo, kwani Biblia yasema kuwa nguvu zote za upapa (mnyama wa kwanza) zitatumwiwa na Marekani (mnyama wa pili) kwa niaba ya upapa. Wataitanguliza ile "sanamu ya mnyama". Hata sasa wameshaanza kufanya hivyo.

### MAREKANI ITAONGOZA KATIKA KULAZIMISHA UTUNZAJI WA JUMAPILI

Wengi watastaajabu watakapoiona Marekani ikiongoza katika kuitanguliza "alama ya mnyama" (shurutisho la kutunza jumapili) na kiisha baadaye nchi zinginezo zitafuata. Wale watakapo wapinga mazimwi hawa (yaani Uprotestanti ulioasi na ukatoliki) na kukataa kuipokea ile "alama ya mnyama" watatiwa alama kama waasi ambao wanahatia ya kuleta misiba na majanga na pia kama wanaoivuruga amani duniani. Biblia yasema kuwa mnamo siku za mwisho amri zitatolewa ili watu hawa wauawe (Ufunuo 13:11-16). Ni wakati huo ambapo Yesu kristo, aliye mwokozi wa dunia, atakaporudi kuwapa uhuru watu wake. (Soma zaidi kuhusu "mnyama mfano wa mwana kondoo" katika kitabu cha Great Controversy kurasa 439 - 445).

### ADHABU KALI

Biblia yadhahirisha wazi kuwa wale watakapoipokea "alama ya mnyama" watapata adhabu ya kuogofya. Biblia hutwambia wazi kuwa wale wanaoipokea hiyo "alama ya mnyama" watakuwa wa kwanza kupitia kwenye maumivu makali wakati wa yale "mapigo 7" yatakayokuja baada ya muda wa rehema kuisha (ufunuo 15: 5-8) Biblia yasema hivi:

# H.R. 2431

## International Religious Freedom Act of 1998

Signed into law  
October 27, 1998  
by the President of  
the United States of America  
William J. Clinton



**“Nikasikia sauti kuu kutoka hekaluni, ikiwaambia wale malaika saba, Enendeni, mkavimimine vile vitasa saba vya ghadhabu ya Mungu juu ya nchi. Akaenda huyo wa kwanza, akakimimina kitasa chake juu ya nchi; pakawa na jipu baya, bovu, juu ya wale watu wenye chapa ya huyo mnyama, na wale wenye kuisujudia sanamu yake.”**  
*(Ufunuo 16:1-2).*

Mapigo sita yanayofuata toka kwenye mabakuli ya hasira za Mungu yatawajia wale walioipokea “alama ya mnyama” huku watoto wa Mungu wakitembea huru (Ufunuo16:1-2) Leo hii, kila mtu hukabiliana na nguvu za shetani za uharibifu. Lakini watoto wa mungu, wanaotambuliwa na mungu, yaani “Mhuri wa mungu”,hawataadhuriwa na yale “mapigo saba”ya mwisho, kama vile Waisraeli hawakudhuriwa na yale mapigo saba kabla yao kuondoka kwenye nchi ya Misri (Kutoka 8:22).

Adhabu ya mwisho,tena baya sana kuwahi kuwajia wale walioipokea “alama ya mnyama”, ni pale ambapo shetani, pamoja na wote waliojitia kwenye upande wake ,watakapo tekelezwa kwa moto na madini ya kiberiti, Biblia yaelezea hivi:

**“Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu**

**yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili”.**  
*(Ufunuo 21:8).*


Wale wote waliompinga mungu watahukumiwa kulingana na matendo yao wakati huo, na watateketea kama vile nyasi wataharibiwa (Ufunuo20:11-15 na Malaki 4:1). Huu ndio uharibifu wa mwisho dhidi ya maovu na wale wote waliokwenye upande wa uovu. Hatimaye mungu ataumba mbingu mpya ambapo haki tu itakayotawala, Nao mviringo huo waishia hapo. Binadamu ataishi peponi aliyoiipoteza-yaani Edeni-pasipo dhambi tena,na ambapo binandamu aweza kunena na mungu uso kwa uso tena, kwani wakati huo atakuwa ameshaupokea mwili wa utakatifu (1wakorintho 15:50-54).

Hili ni jambo la kutazamia, nazo shida za hapa duniani hazitakuwa na umuhimu wowote zikilinganishwa na ule utukufu utakaowajia wateule. Hebu tuombe tupewe Roho Mtakatifu atusaidie kufika pale. Ishara za nyakati zaonysha kuwa saa hii haimo mbali.

### WATEULE WATAENDA MBINGUNI KWANZA

Yesu arudipo, wateule watainuliwa hewani na kupelekwa mbinguni. Haya yaelezwa hivi katika Biblia:

**“Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati**



1) Muhuri wa Mungu:  
Ufunuo 7:2-4  
Ufunuo 14:1-5  
Kutoka 20:8-11  
Ezekieli 9:4

2) Alama ya Mnyama:  
Ufunuo 13:16-17  
Kumbukumbu 6:6-8  
Ufunuo 15:2, 20:4  
Ufunuo 16:2

3) Mwisho wa rehema:  
Ufunuo 15:8  
Ufunuo 22:11

4) Mapigo saba ya Mwisho:  
Ufunuo 15:2-16:21

5) Kurudi kwa Yesu mara  
ya pili:  
Matendo 1:9-11  
Ufunuo 1:7  
Ufunuo 14:14

6) Ufufuo wa kwanza:  
1 Wathesalonike 4:15-18  
1 Wakorintho 15:51-55  
Yohana 5:28-29

7) Wateule pamoja na Yesu  
Mbinguni:  
Ufunuo 6:15-17  
Ufunuo 20:5a  
2 Petro 3:10-12

8) Miaka 1000:  
Ufunuo 20:2-7

**wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafululiwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele..."** (Soma 1 wathesalonika 4:15-17, wafilipi 3:20-21 na Yohana 4:1-3).

Wateule watanyakuliwa hewani pamoja ili wamlaki bwana.

Yesu hataikanyanga dunia wakati huo, lakini wateule watachukuliwa juu angani. Wataelekea Mbinguni (Ufunuo 12)

Biblia yasema kuwa wateule wataishi mbinguni kwa miaka 1000 (Ufunuo 20:4). Hiki kitakuwa ni kipindi cha raha takatifu, tukiwa pamoja na mwokozi wetu yesu, na pia wateule. Lakini pia utakuwa ni muda wa uzito. Biblia yafunua kuwa wateule watahukumu, watahakikisha kuwa wale wasiookolewa wapata hukumu ya haki, na

kuwa Mungu ni wa haki.

Baandayamiaka 1000, wale wasiookolewa watainuka toka makaburini yao na kuipokea hukumu yao ya mwisho. Watatupwa kwenye ziwa la moto lililoelezewa hapo awali.


Kumbuka usome kwa makini mchoro ulio hapo juu!!

### MUNGU AMESHKA USUKANI!

Japokuwa leo yaonekana kana kwamba watawala wa dunia wameitaka dunia, Mungu angali ameshika usukani. Katika wakati umfao, ataingilia kati na kuwa weka huru watu wake, hata awafikishe pahali alipo yaani mbinguni (Yohana 14:1-3). Ndiposa Biblia huyaelezea matokeo ya pambano hili hivi:

**"Kisha nikaona ishara nyingine katika mbingu, iliyo kubwa, na ya ajabu; malaika saba wenye mapigo saba ya mwisho; maana katika hayo ghadhabu ya Mungu imetimia. Tena nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo iliyochangamana na moto, na wale wenye kushinda, watokao**





# MIAKA 1000

- 9) Wateule pamoja na Yesu Mbinguni: Yohana 14:1-3 Ufunuo 20:4, 6 Ufunuo 15:2-4 Ufunuo 7:9-17 1 Wakorintho 6:2-3
- 10) Shetani na malaika zake kufungwa kwa dunia ilio tupu kwa muda wa: Ufunuo 20:1-3 Jeremia 4:23-26

- 11) Ufufuo wa pili: Yohana 5:28-29 Ufunuo 20:5a
- 12) Yerusalemu mpya kushuka: Zekaria 14:3-9 Ufunuo 21:2,10
- 13) Ziwa la moto. Shetani na waovu wote kuangamizwa milele: Ufunuo 20:7-9 Ufunuo 20:13-15 Ufunuo 21:8 Malaki 4:1-4 Isaya 5:24
- 14) Dunia mpya: Ufunuo 21:1-5 Ufunuo 22:1-5 2 Petro 3:11-13

**kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa hesabu ya jina lake, walikuwa wamesimama kando-kando ya hiyo bahari ya kioo, wenye vinubi vya Mungu. Nao wauimba wimbo wa Musa, mtumwa wa Mungu, na wimbo wa Mwana-Kondoo, wakisema, Ni makuu, na ya ajabu, matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi; Ni za haki, na za kweli, njia zako, Ee Mfalme wa mataifa.” (Ufunuo15:2-3)**

Ufunuo 17:14 pia hutwambia kuhusu wale watakaoshinda: awe ni “mnyama” (yaani upapa) na washirika wake, au ni Mwanakondoo” (Yesu) na wale walio katika upande wake. Humalizia kwa kueleza namna hii:

**“Hawa watafanya vita na Mwana-Kondoo, na Mwana Kondoo atawashinda, kwa maana Yeye ni Bwana wa Mabwana, na Mfalme wa Wafalme, na hao walio pamoja naye ndio walioitwa, na wateule, na waaminifu.” (Ufunuo17:14)**

Yesu pamoja na wale wanaosimama upande wake ndiye atakayeibuka mshindi katika pambano lililo mbele yetu. Wale

waaminifu watakuwa na imani ya yesu. Kutokana na upendo wao kwa Mungu, na huku wakiwezesha na Roho Mtakatifu, wataziti amri zake, sio kwa kulazimishwa, bali ni kwa furaha. Biblia husema:

**“Na huko Yerusalemu penye mlango wa kondoo pana birika, iitwayo kwa Kiebrania Bethzatha, nayo ina matao matano. Ndani ya hayo jamii kubwa ya wagonjwa walikuwa wamelala, vipofu, wivete, nao waliopooza, [wakingoja maji yachemke.” (1 Yohana 5:2-3).**

## NANI ATAKAYE KUJIUNGA?

Wale malaika watatu wanaoutangaza ule “ujumbe wa malaika watatu” husimamia binadamu waliojitowa maisha yao kwa kristo. Watautangaza ujumbe huu na inayoeleweka, maana Roho Mtakatifu anashiriki. Je, si wewe pia ungependa kijiunga nasi katika kuutangaza “ujumbe wa malaika watatu?” Sasa wakati umewadia wa kufanya uamuzi huu. Iwapo utajihisi kuwa umefungwa na minyororo ya shetani na pia watawala, mwombe Mungu aliye mbinguni akuweke huru. Biblia hutuhimiza:

**“Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna hii? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira?” (Isaia 58:6)**


Yatupasa wewe na mimi tuombe ili tupewe nguvu za kuivua mizigo yote ambayo dunia imetubebesha mabegani, iliyo pia kinyume na neno la Mungu, hali kadhalika serazinazoambatana na neno hilo. Hujaribu kutufunga na kamba za maelfu ya amri za kibinandamu, hata kutuzuia tusiwe huru katika Bwana. Lakini uhuru wa kweli hupatikana pale tunapoanza kushirikiana na utawala wa mbingu ili tuondoe mzigo wa dhambi. Twakumbushwa pia kuhusu maneno haya ya kutia nguvu kutoka kwa Biblia:

**“Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli.” (Yohana 8:36 walakini alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru.” (2 Wakorintho 3:17)**

KKwa vile twaishi nyakati za mwisho na muda wa rehema u karibu kuisha, yatarajiwa kuwa watu wa Mungu watajithadi kuwaokoa watu toka kwenye mitego aliyoitenga shetani na kuwafungua macho ili wautambue ujumbe wa wokovu. Lakini Biblia hukiita kikundi cha waumini wa nyakati za mwisho “Laodikia” (Ufunuo 3:14-22) Laodikia sifa zake ni uzembe na uvuguvugu. Wengi wa wale ambao hujidai kuamini ujumbe wa malaika watatu ni waumini walio uvuguvugu, wasioonyesha hamu yoyote ya kuwaletea wengine ujumbe huu. Wao si moto au baridi. Hukaa katikati, huku wakijigamba kuwa hawahitaji chochote. Hawataki kuachana na ubinafsi wao. Hujihisi kuwa ni matajiri, wasiokosa chochote cha kiroho, lakini wao ni maskini, vipofu na uchi. Hawawezi kijitambua jinsi walivyo hasa. Je yawezekana kuwa wewe nami tu katika hali sawa na hiyo ya uvuguvugu?

Lakini hebu na tumshukuru Mungu! Yeye hutuonyesha njia ya kutoka kwenye hali hii isiyo na tumaini Hatujui kwa upendo wa moyoni na kutuhimiza tubadilike, tuipokee dawa ya macho anayotukabidhi (Ufunuo

3:18). Dawa hii ni Neno la Mungu likiongelesha dhamiri zetu kupitia kwa Roho Mtakatifu. Tukijipaka dawa hiyo, tutapokea



nguvu za kiroho za kufanya uamuzi utakaotuwzesha kuyastamili mashambulio ya shetani yaliojaa ujanja, pia kuitambua dhambi na kujihisi kuwa kinyume nazo - kuuona ukweli na kuutii. Mabadiliko haya yakishatendeka, Mungu tatutumia tena, na tutakuwa na nguvu za kumshuhudia Mungu katika kazi hii ya mwisho.

Twatumai kuwa utayaweka wakfu maisha yako ili umtumikie Mungu, na ujiunge nasi katika kuutangaza “ujumbe wa malaika watatu” ndani ya maisha yako na katika mafundisho yako. Hili ndilo onyo la mwisho, hali kadhalika ujumbe wa neema kwa ulimwengu ulioanguka, nalo nijukumu la dhati na lenye uzito mwingi lililoezekwa mabegani mwetu. Yatupasa tuelewe ya kuwa twakaribia mwisho wa historia ya dunia hii. Muda wa rehema ukishapita na Yesu kurudi, hapana nafasi nyingine itakayooleana. Sasa ndio wakati ambao yatulazimu kuujibu inavyofaa ule mwito wa Roho Mtakatifu wa kumkabidhi mioyo na mawazo yetu.

Ni ombi letu kuwa watu wengi iwezekanavyo, wanaoyasoma maneno haya, watajihisi kuwa wameitwa washiriki katika kueneza ujumbe huu wa malaika, huku wakijihesabu wemebahatika. Mavuno yako tayari, lakini wafanyi kazi ni wachache, naye Mungu atawatumia wale watakao kuyaweka maisha yao wakfu kwa ajili Yake.

Naomba wewe nami tuwe miongoni mwao!

Salamu za upendo toka kwa

Bente na Abel Struksnes,  
Vestrumsbygda 26,  
2879 Odnes  
NORWAY

[www.endtime.net](http://www.endtime.net)



## **Wanaojabika kukihusu kikaratasi hiki ni Christian Information Service**

*Bente na Abel Struksnes*

*Vestrumsbygda 26, 2879 Odne, Norway*

*au ututumie barua kupitia anwani ya mtandao abels@online.no*

**www.endtime.net**

## **Ni Rahisi na ya kibilia Pokea majubu kwa maswali yako meng BURE!**

"Ukweli wa leo" ni kozi ya Biblia kwa njia ya posta ambayo yaweza kukupa majibu yatakatyokuelekeza kuwa na mtazamo mpya wa dunia hali kadhalika sehemu yako ndani yake Huku Ukilitumia Neno la Mungu pekee, waweza kuugundua ulinzi wake wenye huruma kwa dunia hii na watu wake, na pia SULUHISHO lake ambalo lithushisha ushirikiano wako.

Tafadhali andikia "Ukweli wa leo" P.O. Box 4, Narborough, LEICESTER, LE95XR ENGLAND

### **Vitabu Muhimu!**

"The Great Controversy" na Ellen G White

Waweza kukiagiza kitabu hiki toka kwenye mojawapo ya anwani zifuatazo: "Ukweli wa Leo" P.O. Box 4 Narborough, LEICESTER, LE 9 5XR ENGLAND

Hope International. P.O. Box 940, Eatonville, WA 98328 USA

Fundacion Las Delicias, A.A. 1970 Armenia, Quindio, Columbia Jan Marcussen, P.O. Box 68, Thompsonville, IL 62890, USA

Waweza pia kukiagiza kitabu "The National Sunday Law" toka kwa Jan Marcussen

Kwa habari zaidi za kisasa kuhusu somo hili, tafadhali andikia

#### **David Ngaruyimanzi,**

P. O. Box 14217, Arusha, Tanzania, E.A.

#### **Pr. Livingstone and Margareth Kul Present Truth**

P. O. Box 635, Lae, Morobe Province, Papua New Guinea

#### **Frank Magwano**

Mailbag 18653, Hillbrow 2038, Johannesburg, S.A.

#### **George Kapasa, Back to Eden Ministry,**

P. O. Bag 8, Mkushi, Zambia, C. A

#### **Lily and Sam Ngobi,**

P.O. Box 352, Nhlngano. S400, Swaziland

#### **Isaac Cleon and Bartholomew Poker**

C/o Orlando S. Kanswen, P.O. Box 52, Monrovia, Liberia

#### **Character Building Books**

PO Box 35946 London N17 7WG, England

**giveloudcry@yahoo.co.in**

#### **Meli Tamani**

PO Box A435 Centrepoint, Suva, Fiji.

#### **Correspondence Courses**

47. Mannarino Road. Birkirkara BKR 9082 Malta

#### **The Fiwagoh Missions**

P.O. Box 14390-20100 Nakuru Kenya, East Africa

Nakala zifuatazo hutolewa bila malipo na; Christian Information Service Uhuru Hatarini, Vizuka Vya Mariamu, Pambano Ndani Ya Mawazo na Mfalme Yuaja Kama ungependa kusaidia kuvisambaza vijisuu hivi, tuma barua au barua pepe kwa anwani zifuatazo:

The Fiwagoh Missions P.O. Box 14390-20100 Nakuru Kenya East Africa.  
Email: bekmission@gmail.com +254 722589195





# PAMBANO LILIOFICHIKA

Habari tatu zenye ufunuo  
ambazo zatupatia tumaini  
hata tukiwa tumezingirwa na  
Vurugu...

“Somo la kuisimua! Kipimo kipya huibuka na utaweza kuona pambano kwa mtazamo mpya. Hapa mambo mengi yanapatikana ambayo huwezi kuyapata kwenye vyombo vya habari. Kijisuu hiki kinapendekezwa sana.”

Reggie Wright, Voice in the wilderness